

102/3
KISWAHILI
FASIHI
KARATASI YA TATU
JULAI / AGOSTI 2013
MUDA: 2 ½

MTIHANI WA MWIGO WA WILAYA YA NANDI KASKAZINI 2013

CHETI CHA KUHITIMU MASOMO YA KIDATO CHA NNE

KISWAHILI
FASIHI
KARATASI YA TATU
MUDA: 2 ½

MAAGIZO

1. Jibu maswali manne pekee.
2. Swali la kwanza ni la **lazima**.
3. Maswali hayo mengine yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Riwaya, Tamthilia, Ushairi na Hadithi Fupi.
4. Usijibu maswali **mawili** kutoka sehemu moja.
5. Karatasi hii ina kurasa tano. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI (SWALI LA LAZIMA)

1. (a) Nini maana ya maghani. (alama 2)

- (b) Eleza aina za maghani zifuatazo: (alama 10)
 - (i) Vivugo
 - (ii) Tondozi
 - (iii) Sifo
 - (iv) Tendi
 - (v) Rara

- (c) Taja na ufanue njia za kukusanya data nyanjani. (alama 8)

SEHEMU YA B: RIWAYA

UTENGANO (SAID A. MOHAMED)

Jibu swali la 2 au 3

2. "Mimi nakwenda zangu, lakini tutakapokutana mimi na wewe, ndipo mmoja wetu atakapoona zaidi. Mimi au wewe."
 - (a) Fafanua muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

 - (b) Eleza jinsi ukweli wa usemi huu ulivyojidhihirisha. (alama 6)

 - (c) Msemaji na msemewa wanatofautiana kama ardhi na mbingu. Thibitisha. (alama 10)

AU

3. Eleza matumizi ya mbinu zifuatazo katika riwaya ya Utengano.
 - (a) Chuku (alama 10)

 - (b) Majazi (alama 10)

SEHEMU C: TAMTHILIA

MSTAHIKI MEYA (TIMOTHY AREGE)

Jibu swalii la 4 au 5

4. "Hata Bwana aliteswa kwa sababu ya neno. Mateso yake yalikuwa makubwa. Hayawezi kulinganishwa na tendo hili dogo."

- (a) Fafahua muktadha wa dondo hili. (alama 4)
(b) Eleza ni kwa nini anayeambiwa kauli hili analinganishwa na "Bwana" na ni nani? (alama 2)
(c) Msemaji anazungumzia tendo gani analoliita dogo? (alama 2)
(d) Toa ithibati kuthibitisha ukweli kwamba msemaji na anayeambiwa ni watu wenye sifa za unafiki katika tamthilia ya Mstahiki Meya. (alama 12)

AU

5. Eleza kwa kina sababu zilizochangia migomo katika himaya ya Mstahiki Meya.

(alama 20)

SEHEMU YA D: SHAIRI

6.

Upendo unapovuma, kaskazi kwenda kusi ,
Kwa ngurumu kututuma, ukivisomba vifusi,
Ukasukua milima, nakuyang' oa manyasi,
Ili kukwepa mikosi, miti mikuu hwinama.

Miti mile iloimia , ikaijaza nafasi,
Kwa matawi yake mema, kusheheneza utosi,
Haiwi iko salama, upemo ukenda kasi,
Ili kukwepa mikosi , miti mikuu hwinama.

Upemo ukiivuma , miti haitaanasi,
Huchezeshwa lelemama, ikachezeshwa na dansi,
Matawi yake hunema , yakakatika rahisi,
Ili kukwepa mikosi, miti mikuu hwinama.

Upemo ukitetema, hukata kama makasi,
Miti hwingia ulema, uzima ukawa basi,
Hilivunja tawi zima, kama eawi halinesi,
Ili kukwepa mikosi, miti mikuu hwinama.

Upemo una zahama , hasa ule wa chunusi,
Hata misitu hwandama, ikabaki mufilisi,
Matawi mani huhama, ikapoteza nems,

Ili kukwepa mikosi, miti mikuu hwinama.

Upepo unasukuma, miti hula sarakasi,
Matawi yakachutama, mengi chini hujilisi,
Watu ukiwatazama, wanavua makamasi,
Ili kukwepa mikosi, miti mikuu hwinama.

Ndege wachimachima, viota wameviasi,
Wakajiweka wanyama, kwenye vichaka yabisi,
Majahazi yaparama, yakenda mwemdo wa ngisi,
Ili kukwepa mikosi, miti mikuu hwinama .

Miti mile yenyе kima , yenyе tambo mahsusи,
Mtewi kakikingama, ili upepo kuuasi,
Billahi yaja nakama, kubwa tena kwa wepesi,
Ili kuwepa mikosi, miti mikuu hwinama.

Miti mile hungama, na kujidhili nafusi,
Upepo ukishavuma, ndipo inatanafusi,
Vinginevyo ni kiyama, hapana wa kuramisi,
Ili Kukwepa mikosi, miti mikuu hwinama.

Maswali

- (a) Andika kichwa mwafaka cha shairi hili. (alama 2)
- (b) Eleza ujumbe uliomo katika shairi hili. (alama 3)
- (c) Taja na utoe mifano ya tamathali za usemi zilizotumiwa katika shairi. (alama 4)
- (d) Eleza muundo wa shairi hili. (alama 4)
- (e) Andika ubeti wa sita kwa lugha nathari. (alama 4)
- (f) Eleza maana ya misamiati ifuatayo kama ilivyotumiwa katika shairi.(alama 3)
 - (i) Kututuma
 - (ii) Hitaanasi
 - (iii) Zahama

SEHEMU E: HADITHI FUPI

DAMU NYEUSI NA HADITHI NYINGINE

7. Fikirini ni kielelezo cha mateso wanayopokea waafrika katika nchi za Uzunguni.
Fafanua. (alama 20)

For More Free KCSE past papers visit www.freekcsepastpapers.com